

**MKATABA WA KUPANGISHA SHAMBA LILILOPO KIJJI CHA MTLI –
WILAYA YA MUFINDI**

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe **07 mwezi 07 mwaka, 2021.**

KATI YA

ANDREA P. NGAILO mwenye namba ya simu 0672 759932 ambaye ni msimamizi wa mirathi ya marehemu **THADEI P. NGAILO** wa **MAFINGA**, ambaye katika mkataba huu atajulikana kama mpangishaji kwa upande mmoja.

NA

CHILLI WOOD IMPORT AND EXPORT COMPANY LTD wa **S.L.P 159, MAFINGA** ambaye katika mkataba huu atajulikana kama mpangaji kwa upande mwingine.

AMBAPO, Mpangishaji ni mmiliki halali wa shamba lililopo Mtili "A" lenye ukubwa wa ekari 50(Hamsini) anayo nia ya kupangisha eneo hilo.

NA AMBAPO, Mpangishaji ana nia ya kupangisha shamba hilo na Mpangaji anayo nia ya kupanga shamba hilo kwa shughuli za kibiashara.

Kwahiyo basi Mpangishaji na Mpangaji wanakubaliana yafuatayo:-

1. Kwamba, shamba litapangishwa kwa mda wa miaka mitano kwa shilingi mpangaji za shilingi za kitanzania milioni mia moja (100,000,000/= tu) kuanzia tarehe 01/08/2021 mpaka tarehe 01/08/2026.
2. Kwamba, malipo ya pango yatakuwa yanalipwa kwa mwaka mmoja(1) mara moja yaani shilingi za kitanzania **20,000,000/=(Milioni ishirini tu)** kuanzia tarehe 01/08/2021 mpaka tarehe 01/08/2022.
3. Kwamba, malipo yote ya pango yatalipwa kupitia akaunti ya benki ya mpangishaji ambayo ni
4. Kwamba, gharama za pango kwa mujibu wa mkataba huu zitaanza rasmi kuhesabiwa kuanzia tarehe **01/08/2021**, ili kumwezesha mpangaji kufanya maandalizi ya shamba husika kwa matumizi.
5. Kwamba, mkataba huu unaweza kuhuishwa mara kwa mara kwa mujibu wa makubaliano ya pande zote mbili za makubaliano haya.

6. Kwamba, mpangaji hatakiwi kumpangisha mtu mwingine kwenye shamba bila idhini ya mpangishaji(mwenye shamba).
7. Kwamba, mpangaji hata bughudhiwa katika matumizi ya shamba hilo.
8. Kwamba, kodi au ushuru wa serikali kuhusu matumizi ya shamba zitalipwa na mpangaji.
9. Kwamba, mpangaji anaweza kutoa taarifa(notice) ya kuhama katika kipindi cha siku tisini(90), pia mpangishaji anaweza kutoa taarifa ya maandishi kusitisha mkataba wa upangaji au kutokuwa na naia ya kuhuisha mkataba baada ya mkataba huu kuisha.
10. Kwamba, endapo kutajitokeza tofauti zozote kwa pande mbili kuhusiana na mkataba huu, basi tofauti hizo zitamalizika kwa muafaka kati ya pande mbili na endapo kutatokea kutofikia muafaka upande wowote unaweza kwenda Mahakamani.
11. Kwamba, mkataba unaweza kubadilika kipindi chochote kulingana na majadiliano na muafaka baina ya pande mbili za mkataba huu.
12. Kwamba, mawasiliano au makubaliano yoyote ya ziada yanayoweza kuathiri mkataba huu kati ya pande mbili za mkataba huu, ni sharti yawe ya maandishi na pande zote zitunze kumbukumbu.
13. Kwamba , iwapo utatokea mgogoro wowote basi mgogoro huo utatuliwa kwa Njia ya mazungumzo na kama itatokea kushindwa kufikia muafaka basi sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zitafuatwa.

Mkataba huu umesainiwa na pande zote mbili leo tarehe **07** mwezi **07** mwaka **2021**.

Umesainiwa na kutolewa hapa **MAFINGA**
na **ANDREA P. NGAILO** ambaye
namfahamu binafsi
Leo tarehe **07** ya Mwezi **07** Mwaka **2021**


ANDREA P. NGAILO
.....
MPANGISHAJI

SHAHIDI WA MPANGISHAJI

INA: AMANI NGAILO

SAHIHI: *Pa*
TAREHE: 7-7-2021

Umeshuhudiwa na
Jina VEDASTO P. CHONYA
Sahihi *Pa*
Anuani S.L.P III, MAFINGA
Wadhifa WAKILI



Umesainiwa na kutolewa hapa **MAFINGA**
Na **BAO MU QIANG** kwa niaba ya **CHILLI WOOD**
IMPORT & EXPORT CO. LTD ambaye namfahamu binafsi
Leo tarehe **07** ya mwezi **07** Mwaka **2021**

 Pa
MPANGAJI

SHAHIDI WA MPANGAJI

Jina: **ADRIANI KITINUSA**
Sahihi.....
Anuani.....
Wadhifa.....

Umeshuhudiwa na
Jina VEDASTO PASCAL CHONYA
Sahihi *Pa*
Anuani S.L.P III, MAFINGA
Wadhifa WAKILI

